

Maswali

1. Mbona Mungu alikasirika?
2. Nani alipenda Mungu?
3. Mungu aliamua kufanya nini?
4. Mungu aliambia Nuhu kufanya nini?
5. Mungu alituma nini kwenda kwa Safina?
6. Nani alienda kwa Safina na Nuhu?
7. Nani alifunga mlango?
8. Nini ilifanyika kwa watu waovu wote?
9. Mvua ilinyesha kwa muda gani?
10. Nuhu alikuwa kwa Safina kwa muda gani?
11. Nuhu alifanya nini alipotoka kwa Safina?

Majibu

1. Mungu alikasirika kwa sababu kila mtu alikuwa muovu.
2. Nuhu alimpenda Mungu.
3. Mungu aliamua kuharibu watu waovu wote kwa gharika.
4. Mungu aliambia Nuhu kujenga Safina.
5. Mungu alituma kila aina ya mnyama kuingia kwa Safina.
6. Mke wa Nuhu na wana wake 3 waliingia kwa Safina.
7. Mungu alifunga mlango.
8. Watu waovu wote walizama.
9. Mvua ilinyesha kwa siku 40 mchana na usiku.
10. Nuhu alikuwa kwa Safina kwa zaidi ya mwaka
11. Nuhu alishukuru Mungu kwa kumuokoa yeye na familia yake.
Alipea Mungu mwana kondoo kama zawadi.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 3

2 Nuhu na gharika

Marejeo

Mwanzo mlango wa 6:11 – 22
na milango ya 7 na 8

Kiini cha somo

Kuonyeasha uwamuzi wa Mungu kwa waovu na huruma yake kwa wanaompenda na kumtii.



Maneno maalum

- 2.1 Mungu amekasirika + kila mtu muovu + Nuhu alipenda Mungu + Mungu alitaka upendo na wema + uovu na ukatili tupu
- 2.2 Mungu atagharikisha dunia + Mungu ataokoa Nuhu + jenga mashua
- 2.3 Nuhu alijenga Safina + watu walicheka + Nuhu alimaliza Safina
- 2.4 Mungu alituma wanyama 2 wa kila aina + watu walicheka
- 2.5 Nuhu na familia waliingia kwa Safina + mvua ilianza + waovu wote walizama
- 2.6 Mvua + siku 40 mchana na usiku + Safina ilitua kwa mlima + Nuhu alishukuru Mungu kwa kumwokoa

2.1 Mungu alikasirika sana kwa sababu alipoangalia chini kwa nchi, aliona kila mtu alikuwa muovu. Kila mtu alikuwa muovu ila Nuhu peke yake. Nuhu alipenda Mungu na alijaribu kumfurahisha. Mungu alikasirika na akajuta kwamba alitengeneza mtu na kumweka duniani. Mungu alitaka kuwe na upendo, wema na amani duniani. Badala yake kulikuwa na uovu na ukatili wa kila aina.

2.2 Mungu aliamua kugharikisha nchi yote na watu wote wazame kwa sababu hakutaka kuona hayo maovu yao tena.

Lakini Mungu alimpenda Nuhu kwa sababu alikuwa mtu mzuri na alijaribu kumfurahisha Mungu. Mungu alimwambia kwamba atamwokoia kutoka kwa gharika. Mungu alimwambia Nuhu kujenga mashua kubwa iliyoitwa Safina. Gharika itakapokuja, Nuhu na familia yake watakuwa salama ndani ya Safina.

2.3 Nuhu alifanya vile Mungu alikuwa amemwambia. Alianza kujenga Safina. Nuhu aliishi mbali na bahari kwa hivyo watu walimcheka alipoanza kujenga mashua kubwa vile. Ilimchukuwa Nuhu muda mrefu kujenga hiyo Safina na wakati wote watu walimchekelea. Watu walizungumza maneno yasiyofaa juu ya Nuhu. Hawakuamini kwamba Mungu angetuma gharika nchini. Lakini Nuhu aliendelea kujenga Safina vile Mungu alikuwa amemwambia.

Mwishowe Nuhu alimaliza kujenga Safina. Mungu alimwambia Nuhu achukue aina mbili ya kila mnyama, ndege na mdudu ndani ya Safina ili awaokoe kutoka kwa gharika.

2.4 Mungu alituma kila aina ya wanyama, wadudu na ndege. Wote waliingia kwa Safina mbili mbili. Watu walimchekelea zaidi walipoona akiweka wanyama nao ndani ya Safina. Lakini Nuhu hakujali kwa sababu alikuwa anamwamini Mungu.

2.5 Mungu alimwambia Nuhu aingie kwa Safina. Kwa hivyo Nuhu aliingia na mkewe na familia yake halafu Mungu akafunga mlango na ufunguo. Watu walikuwa bado wanamchekelea Nuhu. Lakini, baadaye anga ilibadilishwa kwa mawingu, kukawa na ngurumo na umeme, watu waliaacha kucheka. Halafu mvua ilianza kunyesha, na watu wakawa na uoga sana.

Walipiga mayowe wakisema, “Nuhu tufungulie!” Lakini Mungu alikuwa amefunga mlango kwa ufunguo, kwa hivyo Nuhu hangeweza kufungua mlango. Walichelewa.

Watu walikimbia kwa nyumba zao mvua ilipoendelea kunyesha. Mvua ilinyesha na kunyesha mpaka maji yakaendelea kujaa na kujaa. Baadaye, paa za nyumba zilifunikwa kwa maji. Watu wengine walikimbia juu ya vilima lakini kwa muda mdogo nazo pia zilifunikwa. Maji yaliendelea kukuja juu, mito zikafurika na mvua iliendelea kunyesha. Mwishowe hata milima mirefu ilifunikwa. Kwa hivyo watu waovu wote walikufa.

2.6 Ilinyesha kwa siku arobaini usiku na mchana ndiyo ikaisha. Watu waovu wote walikuwa wamekufa lakini Nuhu, familia yake na wanyama wote waliokuwa ndani walikuwa hai kwa Safina. Safina ilielea juu ya maji. Baada ya muda mrefu, maji yalirudi chini pole pole. Halafu Safina ilitua juu ya mlima mrefu.

Baada ya muda mrefu nchi ilikuwa kavu tena. Mungu alifungua mlango halafu Nuhu na familia yake na wanyama wote walitoka nje ya Safina. Nuhu alikuwa amekuwa ndani ya Safina kidogo zaidi ya mwaka mmoja.

Nuhu alishukuru Mungu sana kwa kumwokoia yeye na familia yake. Alijenga madhabahu na akatolea Mungu mwana kondoo kama sadaka.